

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA AFYA**



**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA - LIGULA**

**FOMU YA MKATABA WA UKARABATI WA CHUMBA CHA**  
**TELEMEDICINE**

**ZABUNI NA. ME/007/LRRH/2021-22/G/08 11D**

**JANUARI, 2022**

**A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA**

1	<b>Mwajiri</b>	Dr. Lobikieki Kissambu Mganga Mfawidhi Box 520 Mtwara.
2	<b>Jina na anwani ya Fundi (Mwajiriwa)</b>	JUMA SHAHAME, Namba ya simu: 0627788078 Mtwara
3	<b>Eneo la Ukarabati</b>	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Ligula
4	<b>Maelezo ya Kazi kwa Ufupi</b>	Ukarabati wa chumba cha Telemedicine
5	<b>Gharama ya Ufundi</b>	Shilingi Milioni tatu tu (Tsh. 3,000,000/=)
6	<b>Muda wa Mkataba (Tangu Kusainiwa kwa Mkataba):</b>	Tarehe ya Kusaini: 14/01/2022. Muda: Siku 42 (wiki sita) 1. Tarehe ya Kuanza Kazi: Muda wowote baada ya kusaini Mkataba. 2. Tarehe ya Kumaliza Kazi 28/02/2022.
7	<b>Masharti ya malipo:</b>	<ul style="list-style-type: none"><li>• Fundi atalipwa <b>50%</b> ya gharama za ufundi kama malipo ya awali (Advance Payment)</li><li>• Fundi atalipwa awamu <b>pili (45%)</b> baada ya kukamilisha kazi na kukaguliwa.</li></ul>

**B: MASHARTI YA JUMLA YA MKATABA**

1. Mwajiri anakusudia kumwajiri "FUNDI" kwa ajili ya kukarabati chumba cha Telemedicine.
2. Fundi amekubali kukarabati "chumba cha telemedicine" kwa gharama ya Shilingi Milioni tatu tu (Tsh. 3,000,000/=) pamoja na Kodi
3. Mwajiri atatoa vifaa vya (Building materials) vitakavyohitajika kwa ajili ya kukarabati "chumba cha telemedicine" kwa kuzingatia maelekezo ya Msimamizi wa Mradi (Project Manager);



4. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi na Mwongozo wa Msimamizi Mkuu (Project Manager) kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi;
5. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kumtaka kulipa hasara zote zilizotokana na uzembe au makusudi;
6. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na wanakuwa na uaminifu wa hali ya juu. Aidha, ajira za watoto haziruhusiwi kabisa;
7. Fundi atawajibika kwa tabia zote zisizokubalika kama vile wizi, uharibifu wa mali eneo la ujenzi na vitendo vyote vitakavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake. Aidha, atawajibika kwa kutoa fidia kwa watumishi wake ikiwa watapata ajali kazini;
8. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia atakapomaliza kazi, ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la usimikaji kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama;
9. Kiasi cha asilimia tano (5%) ya kiasi cha Mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa mwezi mmoja baada ya kazi kukamilika (*Retention Money*) na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho wa pamoja kufanyika na pale itakapoonekana kuna marekebisho yatafanywa kwa gharama za fundi;
10. Fundi anatakiwa kuwepo eneo la usimikaji muda wote wa utekelezaji wa mradi;
11. Fundi anatakiwa kuandaa mpango kazi na kuuwasilisha kwa mwajiri wakati wa utekelezaji wa mradi na anatakiwa kuufuata ipasavyo;



12. **Ucheleweshaji wa Kazi:**

- **Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi**, fundi atalipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo;
- **Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwijiri** (kutokana na fedha au vifaa), Fundi ataongezewa muda sawa na kipindi chote kazi iliposimama;

13. **Uvunjwaji wa Mkataba:**

Mkataba utavunjwa iwapo;

- Fundi au mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya eneo la ujenzi.;
- Fundi au fundi msaidizi hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya *Project Manager* ambaye ni Mhandisi wa Mkoa;
- Fundi akichelewesha kazi kwa muda wa mwezi 1 bila sababu yoyote ya msingi.


**MWAJIRI:**

Jina LOBIKICIA KIMAMBU

Saini [Signature]

Cheo: MGANGA MPAWIDHI

Tarehe 14/01/2022



**SHAHIDI WA MWAJIRI**

Jina FALU MEWA

Saini [Signature]

Cheo: AFISA UGAVI

Tarehe 14/01/2022


**FUNDI:**

Jina JUMA HAMIS SHAHANE

Saini [Signature]

Cheo: FUNDI

Tarehe 14/01/2022



**SHAHIDI WA FUNDI**

Jina ARAKH H. SHAHANE

Saini [Signature]

Cheo: FUNDI

Tarehe 14-1-2022